Mafundisho Si Neno Baya

na

Terry Warford

Mafundisho Si Neno Baya

na

Terry Warford

Novemba 5, 2011

Mafundisho Si Neno Baya

Katika 1 Tim. 4:13, tunasoma, "*Hatanitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha.*" Na mustari wa 16 unaendelea, "*Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.*"

Mafundisho ni kitu ambacho tumeamriwa kukifanyia bidii na kusikiliza. Kukishikilia itasaidia kutuokoa na wale wanaotusikia. Kwa kawaida hiki ni kitu ambacho ni muhimu, sana.

Vile vile katika mzunguko mwingi wa kidini wazo la mafundisho, ukweli, na sheria za kufuata karibia inachukuliwa kama wazo ambalo si safi. Kitu pekee ambalo linasemwa katika swala hili ni uaminifu na bidii. Kujaribu kufanya mambo sahihi ni kulaumiwa kwa kutokuwa mwaminifu, pia kiufundi na uwazi.

Hakuna mtu aliyekuwa tayari kuniuzia kiwango hicho cha mali. Na nina tarajia tunapojifunza pamoja, kwamba wewe pia, utaona umuhimu wa mafundisho yetu.

Kwanza, hebu na tunyumbulishe kile ambacho Biblia inamaanisha kwa neno maandiko. Katika Marko 1:21-22, tunasoma hili kuhusu Yesu, "*Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi* (Yesu) *akafundisha. Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi.*"

Kile ambacho Yesu alifundisha kiliitwa mafundisho yake. Hayo ndiyo yote tunayosema tunapotamka fundisho hilo ni muhimu. Kirahisi tunasema kwamba kile ambacho Yesu alifundisha ni muhimu. (Hiyo itawezaje kutufanya tusiwe waaminifu ni zaidi yangu).

Kwa kweli, kuna mafundisho ya kupotosha pale nje pia, ambayo tunatakiwa kuwa makini nayo. Math. 15:8-9, "*Watu hawa huniheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*" Mafundisho ya kweli ni ile ambayo Yesu alifundisha. Mafundisho ya uongo ni maagizo ya wanadamu.

Hivyo, tunawezaje kuwa na uhakika kwamba mafundisho tunayofundisha ni kile ambacho Yesu Kristo alifundisha, si mwanadamu?

Mwanzo wa yote, kumbuka kwamba tunasoma hapo juu (Marko 1:22) kwamba mafundisho yake yalikuwa yenye mamlaka. Yesu alipatawapi mamlaka haya? Aliyapata kwa Mungu.

Yohana 7:14-16, "*Hata ikawa katikati ya sikukuu Yesu alikwea kuingia hekaluni, akafundisha. Wayahudi wakastaajabu wakisema,*

Amepataje huyu kujua elimu, ambaye hakusoma? Basi Yesu akawajibu, akasema, mafunzo yangu si yangu mimi, ila ni yake yeye aliyenipeleka."

Yesu, alafu, akawapa wanafunzi wake mamlaka. Kumbuka kile alichomwambia Petro katika Math. 16:19, "*Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lo lote utakalo lifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*"

Si kwamba tu alimpa Petro na mitume wengine mamlaka ya kufunga na kufungua vitu vya ufalme. Bali pia aliwafundisha vitu vya kufunga na kufungua. Matendo 1:1-3, "*Kitabu kile cha kwanza nalikiandika Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha. Hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua; wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini na kuyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu.*"

Mitume alafu wakafundisha kile ambacho Kristo aliwafundisha, na kuliandika chini ili kwamba tuwe nayo leo. 2 Petr. 3:1-2, "*Wapenzi waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi katika zote mbili naziamsha nia zenu safi kwa kuwakumbusha, mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu na ile amri ya Bwana na Mwokozi iliyoletwa na mitume wetu.*"

Mafundisho yetu yote yaliandikwa na mitume, na tunaweza kuyasoma. Kwa neema ya Mungu iliyotolewa kupitia Yesu Kristo kwa baraka nyingi ambazo tume barikiwa nazo leo, kwa njia tunayo paswa kuwahudumia wengine, kwa kiwango chetu, kwa jinsi tunavyopokea neema yake, na ndiyo katika ibada yetu na katika kweli. Yote yameandikwa. Tunaweza kuyasoma yote. Kutegemea **Siyo** ustadi au ubora. Ni kunyenyekea kwa kutii, kujikabidhi kwa Mapenzi ya Mungu.

Mtume Paulo aliandika mengi kuhusu neema, shauku, na uaminifu. Pia ni yeye aliyetaja utii kwa mafundisho ya Kristo siyo ma-neema bali sehemu ya neema yake. Kumbuka Waru. 6:15-17, "*Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? Hasha! Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliiti kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake.*" Tunataka kuangalia vipengele vitatu katika mistari hii.

Kwanza, ni mafundisho ya aina gani waliyopewa? Kile ambacho mitume walitoa. Mitume walipokea kutoka kwa Kristo, ambaye alipokea

kutoka kwa Mungu. Mafundisho hayo hayo yalitolewa kwetu kupitia maandishi ya mitume.

Kipengele cha pili, tunaweza kuitii dhambi, au tunaweza kutii mafundisho yanayotoka kwa Yesu Kristo. Lakini usifanye kosa. Tunatii kitu. Tunatii mmoja baada ya mwingine.

Tatu, kwa nini tulitii hiyo namna ya elimu (ndiyo, mafundisho) ambayo ilitolewa kwetu? Tulitii ili tuwe na ustadi, kutoka katika uaminifu? Au tulitii bure? **Hapana!** Paulo alisema tulitii kutoka moyoni.

Sasa kwa nini usimtii Mungu? Kwa nini usitii namna ya elimu ambayo mitume walipokea kutoka kwa Yesu? Kwa nini tusinyenyekee chini ya mikono ya Mungu?

Kwa nini uongeze vitu katika mafundisho ya Yesu ambayo hakuamuru? Vitu vingi vimeongezwa kwa kile ambacho Yesu na mitume wake walifundisha. Yaliongezwa na wanadamu. Je sisi tuna upeo kuliko Mungu? Je njia zetu ni nzuri kuliko zake?

Kwa nini usijikabidhi kwa Yesu?

Nafikiri kipeperushi hiki inaonekana kama kinga. Hicho si kitu ambacho nilitarajia. Lakini, unajua nini? Wakati mwingine mafundisho yetu (na nia yetu katika mafundisho haya) inafaa kutetewa.

Watu wanapokushutumu kwa kutokuwa muwazi au mwaminifu, usijali. Hawawezi kusoma mawazo yako, hawana haki ya kuhukumu kile ambacho kipo katika moyo wako. Hawajaribu kujipendekeza wenyewe kwa kufanya ambacho Biblia inasema. Wanajaribu kujipendekeza wenyewe kwa kutushambulia.

Kutaka kumtii Mungu si kithibitisho cha kutokuwa mwaminifu. Ni kithibitisho cha uaminifu, unyenyekevu na hamu. Ni namna ya uaminifu ya utukufu na kutoa shukurani.

Waru. 6:13, "*Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki.*"

Katika Upendo wa Kristo,

Ndg. Terry Warford